JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## MABADILIKO YA TAREHE YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI KWA MWEZI WA MEI, 2023

Mnatangaziwa kuwa siku ya kufanya ya mtihani wa Usajili na leseni imebadilishwa kuwa tarehe **25/05/2023** badala ya tarehe iliyokuwa imetajwa hapo awali. Aidha, watahiniwa walioomba kufanyia mtihani katika kituo cha **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu (DUCE)** watafanyia mtihani katika kituo cha **Chuo cha Uuguzi na Ukunga Lugalo.** Mtihani huu ni kwa wahitimu wote waliofuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga na kupata sifa ya kufanya mtihani kwa ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada pamoja na wale wanaorudia mitihani hiyo.

**Orodha ya Vituo vya Mitihani vitakavyotumika ni kama ifuatavyo;**

| SN | Kituo | Mkoa |
|---|---|---|
| 1 | Tandabui - Taasisi ya Afya Sayansi na Teknolojia | Mwanza |
| 2 | Chuo cha Uuguzi na Ukunga Lugalo | Dar es Salaam |
| 3 | Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji | Mbeya |
| 4 | Chuo Kikuu cha St. John | Dodoma |

Maombi ya mtihani yanapokelewa rasmi kwa njia ya mtandao kwa kutumia mfumo wa Baraza **https://tnmcis.tnmc.go.tz** kuanzia tarehe **27/03/2023** hadi tarehe **10/05/2023.** Kila

Jengo la Kambarage Tower, Ghorofa ya 5, Barabara ya Benjamini Mkapa, S.L.P 1736, DODOMA Simu: +255262966061/62/63, +255737 962 691, Barua pepe : info@tnmc.go.tz, Tovuti : www.tnmc.go.tz

mtahiniwa atatakiwa kujaza fomu ya maombi (softcopy) na kulipia Shilingi 150,000/- kwa wanaoomba kufanya mtihani huu kwa mara ya kwanza na Shilingi 75,000/- kwa wanaorudia mitihani hiyo. Watahiniwa wanaorudia wanashauriwa kuomba mtihani kwa kutumia akaunti zao za awali.

Mnakumbushwa kuzingatia taratibu zote za maombi ambazo zimeainishwa kwenye mwongozo wa maombi ya mtihani wa Usajili na Leseni ambao unapatikana kwenye tovuti ya Baraza www.tnmc.go.tz ikiwemo;

- Kuweka picha sahihi (passport size) yenye kivuli cha blue, **HD** ukubwa **35x35 mm (Isiwe picha ya kupigwa kwa kutumia camera ya simu za mkononi)**
- Kujaza majina sahihi kama yalivyo andikwa kwenye cheti chako cha **kidato cha nne.**

**NB.** Watahiniwa watakao kiuka vigezo na taratibu za kuomba mtihani, maombi yao hayatapokelewa.

Nawatakia maandalizi mema.

Jane Mazigo
**Kny: MSAJILI**

**20/04/2023**

Jengo la Kambarage Tower, Ghorofa ya 5, Barabara ya Benjamini Mkapa, S.L.P 1736, DODOMA Simu: +255262966061/62/63, +255737 962 691, Barua pepe : info@tnmc.go.tz, Tovuti : www.tnmc.go.tz